# Kisiwa cha Migingo: Diskosi Tepetevu

*Samuel M. Obuchi*[1] na *Nabeta K. N. Sangili*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Moi, Kenya*
[2]*Chuo Kikuu Kishiriki cha Kaimosi, Kenya*

**Ikisiri**

**Makala haya yanaangaza diskosi tepetevu kama inavyojitokeza katika lugha iliyotumiwa na viongozi mbalimbali wa Afrika Mashariki kuhusiana na umiliki wa kisiwa cha Migingo. Wandishi wanajadili matumizi ya lugha ya viongozi hawa, hususan Rais Yoweri Museveni ambaye alidai kwamba pasina shaka, kisiwa cha Migingo kipo chini ya himaya ya Kenya ila maji yanayokizunguka yanamilikiwa na Uganda. Baadhi ya viongozi kutoka Uganda walidai kwamba hapakuwa na sababu ya upande wa Kenya kung'ang'ania mwamba au jiwe lisilozidi kipimo cha uwanja wa mpira. Matamshi haya yalizua mjadala mrefu sana kuhusiana na umiliki wa kisiwa hiki huku pande mbili zinazohusika zikishikilia misimamo mikali ambayo, pasina shaka yoyote, ingesababisha kutoelewana na pengine, machafuko ya kisiasa. Katika makala haya, tunauangazia mgogoro huu ndani ya nadharia ya Diskosi Hakikifu Changanuzi (DHC). Katika kufanya hivi, tutajaribu kuonyesha namna mamlaka na nguvu za kisiasa na kijamii huongoza maingiliano yanayohusu mataifa yanayozozania kipande fulani cha ardhi.Van Dijk (1998) anafafanua Diskosi Hakikifu Changanuzi kama mtalaa unaoshughulikia uhakiki wa matini ama iliyoandikwa au inayosemwa, kwa lengo la kutambua vianzo vya mamlaka, utosawa, na amri juu ya upendelevu. DHC huchunguza namna hali mbalimbali za mamlaka huhifadhiwa na kuendelezwa katika miktadha mahususi ya kijamii, kisiasa na kihistoria.**

**Maneno Muhimu:** *Diskosi, Mgogoro, Tepetevu, Siasa, Migingo*

## Utangulizi

Kwa mujibu wa Van Djik (1998) katika Obuchi na Sangili (2016), DHC ni nadharia inayoshughulikia uchambuzi na uhakiki wa matini, ilioyoandikwa au iliyosemwa, kwa lengo la kutambua vianzo vya mamlaka, utosawa na amri juu ya upendelevu uliomo katika jamii. Diskosi hii huchunguza udhihirikaji wa mamlaka katika asasi na maingiliano mbalimbali, ya kisasa na ya kihistoria. Nadharia hii imeweza kujitokeza katika taaluma ya fasihi. Diskosi hii pia hushughulikia masuala ya urasimu, na harakati za kikazi (Brown& Yule, 1983; Bauman & Sherzer, 1984). DHC pia huchukuliwa kama aina ya uhakiki wa diskosi unaolenga kuelezea uhusiano usio wa moja kwa moja

kati ya hali na shughuli mbalimbali za kijamii. Katika hali hii, Diskosi hii hulenga katika kuchunguza na kuhakiki:

(i) Mahusiano ya kimfanyiko yanayojitokeza katika miktadha mbalimbali, matukio na matini.
(ii) Namna mifanyiko, matukio na matini zinavyokutana na mielekeo ya kiitikadi inayoendana na mahusiano ya kimamlaka na mashindano ya kimamlaka.
(iii) Miundo mipana ya kijamii na kitamaduni inayobainisha mahusiano ya kimamlaka kati ya washirika mbalimbali katika jamii.
(iv) Kubainisha mahusiano ya kimamlaka yaliyofichama ndani ya jamii kwa minajili ya kukuza maelewano.

Kwa ufupi, DHC huweka wazi uhusiano kati ya mifanyiko ya kidiskosi, ya kijamii pamoja na miundo ya kijamii ambayo, mara nyingi, haijitokezi waziwazi kwa msomaji au msikilizaji wa kawaida. Diskosi hii ni eneo lenye historia inayorudi nyuma hadi miaka 70, na ilitokana na kundi la wanaisimu pamoja na wananadharia wa kisanaa (Fowler *na wenzie,* 1979; Kress na Hodge, 1979). Kwa mujibu wa Obuchi na Sangili (2016), nadharia hii ilikitwa kwenye mtazamo wa sarufi amilifu ulioasisiwa na Halliday. Waasisi wa DHC waliegemeza maono yao kwenye mwelekeo wa Halliday, huku wakiangalia matumizi ya lugha kama yanayotekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Uamilifu wa kiutambuzi na jinsi ya kufikiri.
(ii) Mahusiano kati na baina ya watu.
(iii) Uamilifu wa kimatini.

Uhusiano wa kiutambuzi hurejelea tajriba ya msemaji kuhusu ulimwengu na malimwengu yake. Hii ina maana kwamba matendo yetu ya kila siku, semi zetu za kila mara na yale tunayoyasoma kila wakati huvyaza jinsi tunavyotazama na kuwazia ulimwengu wetu. Kwa upande mwingine, mahusiano kati na baina ya watu yanarejelea uhusiano baina ya wanajamii; huangalia mielekeo ya msemaji na tathmini yake kuhusu vipengele fulani kwa lengo la kukuza na kuimarisha uhusiano kati ya wasemaji na wasikilizaji. Uamilifu wa kimatini hurejelea namna wasemaji huzalisha matini zinazoeleweka kwa wasikilizaji. Katika hali hii, lugha hutazamwa kama tendo la kijamii na, hivyo, kuwa na uhusiano wa karibu kati ya miundo ya kiisimu na miundo ya kijamii. DHC huangalia pia namna wasemaji au watumiaji wa lugha hufanya uteuzi wao wa msamiati na mbinu zingine za lugha kwa kupanga. Uteuzi huu huwa unaongozwa na itikadi maalumu inayotawala jamii. Mtazamo wa DHC hulenga katika kufasili matini, kando na kutekeleza jukumu la kuhakiki na kufafanua matini za sampuli mbalimbali. Kipashio cha uchunguzi katika taaluma ya DHC ni matumizi ya lugha katika miktadha na mazingira halisi ya kimaingiliano. Maumbo haya ya lugha huchunguzwa kwa kurejelea namna yanajitokeza na kutumiwa katika miktadha mahususi ya kijamii, kwa mfano matangazo ya kibiashara na ukuzaji wa utamaduni, masuala ya kiuana/kijinsia na uwakilishi wa wanawake katika taaluma ya Kisiasa (Talbot, 1992; Caldas-Coulthard, 1993; 1996), na lugha ya vyombo vya habari (Fairclough, 1995; Van Dijk, 1991; Kress, 1994).

Katika siku za hivi karibuni, kumetokea haja ya kupanua mawanda ya uchunguzi unaovuka mipaka ya matini kwa kuiendeleza kwenye isimu matini. DHC basi, ni mtazamo wa kinadharia unaofungamana na mawazo ya taaluma mbalimbali. Diskosi hii si nadharia mahususi inayojitegemea, bali ni mtazamo ambao unajumuisha mawazo na mielekeo kutoka taaluma nyingine nyingi kama vile anthropolojia, saikolojia, sosholojia nakadhalika. Miongoni mwa wataalamu ambao wamechangia nadharia hii ni pamoja na van Dijk (1998), wodak (1996) na Fairclough (1999). Wataalamu hawa wanatofautiana kwa kiasi kikubwa kwa sababu kila mmoja ana mwegemeo, msisitizo na itikadi zinazomtawala. Ni katika mkabala huu wa mawazo ambapo lugha na itikadi hujiri kama mada kuu katika DHC (Van Dijk, 1998). Hapa, Diskosi hujitokeza kama njia ya kukuzia na kuendelezea itikadi fulani (Obuchi & Abdulaziz 2009, Obuchi 2010, 2011) . Hata hivyo, Nadharia ya DHC imechunguzwa, kwa kiasi kikubwa, na wanaisimujamii na wanaisimu kianthropolojia. Hata hivyo, mabadiliko katika jamii za kisasa yanasababisha DHC kupanuliwa na kuingizwa katika miktadha ya siasa za kimaeneo kama vile mzozo uliopo kati ya Kenya na Uganda kuhusu kisiwa cha Migingo.

## Chanzo cha Mgogoro

Magazeti ya Afrika mashariki (*Daily Nation,* 2008, 2009; *Daily Monitor,* 2008) yanatupa fununu kuhusu chanzo cha mgogoro huo. Magazeti haya yanadai kwamba Wavuvi wawili Wakenya, Dalmas Tembo na George Kibebe, wanadai kuwa wenyeji wa kwanza kwenye kisiwa hicho. Wakati walipofika huko mwaka 1991, kisiwa kilikuwa kimefunikwa na magugu na kimejaa ndege na nyoka. Yusufu Nsubuga, anasema alifika huko mwaka 2004, wakati hakukuwa na kitu ila nyumba iliyoachwa. Hatimaye, wavuvi wengine - kutoka Kenya, Uganda na Tanzania - walikuja kwa sababu kisiwa kilikuwa karibu na maeneo mazuri ya uvuvi wa samaki. Madai yasiyo ya kawaida ya mwaka 2009 na baadhi ya wavuvi wa Kenya yalikuwa kwamba kwa kuwa samaki huzalishana kwa wingi nchini Kenya, basi samaki hao ni "mali ya Wakenya".

Juni 2004, kulingana na serikali ya Kenya, polisi wa maji wa Uganda walikuja wakatua kisiwani na kupandisha bendera ya Uganda na ya idara ya polisi. Polisi wa Uganda na Kenya wamekuwa katika kisiwa hiki katika nyakati mbalimbali. Mgogoro ulizuka Februari 2009 wakati Wakenya wanaoishi Migingo walikuwa wakitarajiwa kununua vibali maalumu kutoka serikali ya Uganda, hivyo kusababisha mgogoro wa kidiplomasia kati ya nchi hizi mbili. Kenya na Uganda zinapaswa kuondoa wasiwasi na kutafuta suluhu la kidiplomasia kwenye mgogoro wao wa muda mrefu kuhusiana na mipaka iliyopaswa kuyatenganisha mataifa haya ya Afrika Msharikí. Mzozo huu kwa hakika unahusu haki ya uvuaji wenye thamani, lakini lilikuwa tukio la tarehe 30 Juni wakati wanachama wa kikosi cha polisi cha Uganda kilipodaiwa kuwapiga na kuwajeruhi maofisa wa polisi wa utawala wa Kenya huko Migingo. Tukio hili kwa muda mrefu liligonga vichwa vya habari katika mataifa haya.

Vyombo vya habari vinaripoti kuwa tukio hilo liliibuka wakati maafisa polisi kadhaa wa Uganda walioweka kambi huko Migingo walipoondoka kwenda Nyandiwa,

Kenya. Maafisa hao walidaiwa kusimamishwa na maafisa wa polisi wa utawala kutoka Kenya ambao walisema kwamba walitakiwa kusajili silaha zao kabla ya kusafiri kwenye maji ya Kenya. Ombi hilo lililotolewa liliwaudhi maafisa wa Uganda ambao walilipiza kisasi dhidi ya maafisa polisi wa Kenya waliokuwa wamekita kambi karibu na kisiwa cha Ugingo waliposafiri kwenda Migingo kununua chakula.

Mjadala mpevu uliendelea kushamiri kati ya viongozi wa pande zote mbili kuhusiana na madai kwamba kulitokana na "kuelewa visivyo" matamshi fulani ambayo hayakukusudiwa kuhujumu utulivu na amani kati ya nchi hizi mbili. Viongozi wa pande zote mbili waliendelea kudai kwamba mgogoro huo ulisababishwa na kukatika kwa mawasiliano. Majaribio haya ya kutuliza hali hiyo huko Migingo yalisaidia kwa kiasi kidogo kupunguza shinikizo kutoka kwa umma na wabunge kutoka pande zote mbili. Ni kutokana na hali hii ambapo Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta, aliamua kutochukua hatua za kuiadhibu Uganda, japo baadhi ya Waganda wameliita tukio la Migingo kuwa ni shambulizi dhidi ya uhuru kamili wa nchi yao.Wakenya walipendelea amani, na kukumbatia juhudi za kuendeleza hali ya ushirikiano na Uganda. Waganda wengi walionelea kuwa kuna haja kwa Wakenya kupunguza malumbano ya kisiasaambayo yangesababisha maafa makubwa kwa pande zote mbili. Masuala yanayogusa sheria za kimataifa, uraia na muungano wa kanda ni masuala yenye uzito mkubwa. Masuala haya yanahitaji tahadhari, la sivyo, yanaweza kuchochea vita au migogoro ya kiuchumina kisiasa katika maeneo ya Afrika Mashariki.

Inavyobainika ni kwamba matumaini ya kufikia maazimio ya kirafiki katika nchi hizi mbili yalipaswa kuchapuza jitihada za kutatua mgogoro huo. Mbinu ya kurejesha nyuma ya serikali ya Kenya inaleta wasiwasi kwa sababu, ilikisiwa, inachangia katika kutoridhika kwa mataifa haya kuhusiana na suala hili. Kwa kweli, rais wa Uganda alielekea kuendeleza hali tatanishi na hivyo kuendeleza mgogoro huo kinyume na hali ilivyoelekea kujitokeza nchini Kenya ambapo rais alielekea kuchukua tahadhari dhidi ya ugomvi. Kwa kweli, hii ni mbinu ya Rais Kenyatta kuuvutia tafakuri mgogoro huo kwa ajili ya kusubiri suluhu la kudumu. Ifahamike kuwa Rais Uhuru aliwaahidi Wakenya wakati wa kampeni zake kuwa angekirejesha kisiwa cha Migingo endapo angechaguliwa kama Rais. Baada ya kuchaguliwa, Uhuru alisema Kenya inaweza kuutanzua mgogoro wa Migingo na Uganda kwa njia za amani na kuepuka msuguano wa kijeshi.

Mgogoro unaweza kutokea kutokana na vitendo vizuri katika migogoro ya baadaye kuhusu mipaka miongoni mwa nchi wanachama wa Afrika Mashariki. Inaweza pia kutoa namna nzuri ya kupima maandalizi kwa ajili ya udanganyifu mkubwa kuvuka kwa uhuru mipaka ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa, watu na huduma. Kwa kuzingatia takwimu za Taasisi ya Utafiti wa Rasilimali za Uvuvi ya Taifa la Uganda na Tume ya Takwimu ya Kenya, Uganda ilizalisha tani za ukubwa 70,061 za sangara wa Nile mwaka 2011, ambapo Kenya ilifanikiwa kuzalisha tani 111,619. Hivyo, kutokuwa na uwiano na kupunguza rasilimali za samaki katika ziwa ambalo ndio sababu kuu ya mgogoro wa Migingo. Kwa miongo sasa, Kisiwa cha Migingo kilitambuliwa kama sehemu ya himaya ya Kenya, lakini mwaka 2008, serikali

ya Uganda ilidai kisiwa hicho. Hilo lilibadilika mwaka mmoja baadaye wakati Rais wa Uganda Yoweri Museveni alipodai kwamba kisiwa kilikuwa cha Kenya, bado alidai maji yaliyopo karibu yalikuwa ni sehemu ya Uganda. Tarehe 13 Machi mawaziri kadhaa wa serikali, pamoja na mawaziri wa masuala ya kigeni - Moses Wetangula kutoka Kenya na Sam Kutesa kutoka Uganda - walikutana mjini Kampala, Uganda na kufikia makubaliano kwamba wavuvi kutoka nchi zote kuruhusiwa kuendelea kufanya biashara kama kawaida, mpaka eneo rasmi lidhamiriwe na wataalam. Pia walikubaliana kuwa Uganda waondoe polisi arobaini na nane waliokuwa wametuma katika Migingo.

Tarehe 27 Machi mawaziri wa Uganda na Kenya walifika kisiwani ambapo waliafikiana kuhusu masuala mbalimbali yaliyowahusu wakazi wa kisiwa hicho. Hata hivyo, kulitokea mtafaruku fulani kwani Naibu Waziri Mkuu wa kwanza wa Uganda, Eriya Kategaya alikasirishwa na Waziri wa Ardhi wa Kenya, James Orengo, kwa kuwaita wa Uganda "mafisi" wakati wa mkutano. Balozi wa Uganda alisisitiza kwamba wangetoa bendera tu baada ya kuishauri Ofisi ya Rais wa Uganda, na kwamba polisi wa Uganda walikuwa na jukumu la kuandaa ratiba ya kuongoza shughuli hiyo. Naibu waziri wa usalama wa Kenya, Orwa Ojode, alijibu kuwa angetuma polisi wa Kenya katika kisiwa hicho. Katikati mwa mgogoro wasiwasi kuwa kunaweza kuathiri ushirikiano kati ya nchi hizi mbili na ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, wote Museveni na Rais Mwai Kibaki wameonyesha nia na uwezekano wa mgogoro, pamoja na changamoto zinazoendana na haki za uvuvi, kutatuliwa kirafiki.

> Kenyans want to express their feelings of frustrations and anger over the issue of Uganda’s unexplained boldness and belligerence, and our own government’s apparent feeble response to the issue. This explains the robust behaviour of Kibera residents over Migingo Island and other issues they have voiced concerns over.

Mzozo wa migingo unafungamana na diskosi ya uhaba wa rasilimali. Uganda basi ikakivamia kisiwa hiki ili kupata nafasi nzuri ya kumiliki na kuendesha shughuli za uvuvi. Katika mwaka wa 2008, ambapo Wakenya wasiopungua 400 walihitajika kulipa shilingi elfu hamsini za Kenya kama ushuru ulioendana na shughuli za uvuvi kule kisiwani. (The East African, 22/11-2008, Daily Monitor, 27/10-2008). Juhudi za kidiplomasia kutoka upande wa Kenya ziliambulia patupu. Vyombo vya habari kutoka Kenya zikaripoti kwamba kulikuwa na haja ya kulinda, sio tu usalama wa taifa, bali pia uhuru (*Daily Nation*, 1/5-2009), kuwapeleka askari wake kule Migingo.

Kilichozua wasiwasi zaidi ni kuwepo kupeperushwa kwa bendera ya Uganda katika kisiwa hicho, japo mataifa hayo mawili yalikuwa yameafikiana kuwa Uganda ingeyaondoa majeshi yake kutoka kisiwa hicho. Akiwahutubia umati uliofika kuhusiana na mtafaruku huo, aliyekuwa waziri wa ardhi James Orengo alisema kwa lugha ya Dholuo (hapa tuna tafsiri) kwamba: “Stay calm, diplomacy shall overcome force, and we will have our way”. Bwana Orengo hakufahamu kwamba dholuo ni mojawapo ya lugha zinazosemwa nchini Uganda na la ajabu ni kwamba idadi ya jamii ya waluo nchini Uganda inazidi ile iliyoko nchini Kenya. Aidha, waziri

anayewaakilisha waluo nchini Uganda ni Mjaluo aitwaye Henry Ochieng ambaye anawaakilisha eneo ambalo lina wabantu wengi kuliko waluo! Lakini wajumbe kutoka Uganda walikasirishwa na matamshi ya waziri huyo, wakisema kuwa wanaifahamu vyema lugha ya Kijaluo. Eti Orengo alikuwa akiwachochea Wajaluo. Ndipo walisimama na kufumukana. Mazungumzo hayo yakasambaratika.Wakenya kwa upande wao wakashikilia kuwa kupeperushwa kwa bendera ya Uganda kulielekea kuwa na maana ya kisiwa hiki kuwa mali na milki ya waganda. Ndipo mjumbe kutoka Uganda Kirunda Kivejinja akatamka kuwa Uganda itaondoa bendera yake kutoka kisiwa hicho kinachozozaniwa baada ya kupata ushauri kutoka Ikulu ya Uganda. Walipoulizwa kwa nini hawakuwa wameondoa askari wake kutoka kisiwa hicho, walijibu kuwa walikuwa wakiimarisha usalama na utulivu. Ndipo Waziri msaidizi wa masuala usalama wa ndani Orwa Ojode, aliposema kuwa atatuma askari polisi wa Kenya katika kisiwa hicho. Kuna uwezekano kuwa katika siku za hivi karibuni, vita vya aina yoyote katika maeneo mbalimbali ulimwenguni vitasababishwa na uhaba wa maji.

**Migingo: Diskosi Tepetevu**

Pengine kabla ya kuzama zaidi katika mjadala, ni vyema kuweka wazi hali halisi kuhusu historia fupi ya mgogoro wa Migingo kati ya Kenya na Uganda. Kwa mujibu wa AFP (2008/2009) kisiwa cha Migingo kilianza kuzozaniwa mwaka wa 2008 wakati ambapo wavuvi wa Kenya walishikwa na askari wa Uganda kwa madai ya kuvua samaki katika maeneo ya Uganda. Hata hivyo, shirika la wanahabari la Reuters linadai kwamba askari wa Uganda ndio walikuwa wa kwanza kuweka makao yao kwenye kisiwa hicho mwaka wa 2004 licha ya kwamba ni sehemu ya Kenya. Hali hii ilizua mgogoro uliodumu kwa muda mrefu na kulipuka mwaka wa 2008 Rais Kibaki alipokuwa katika hatamu zake za mwisho kama Rais wa Kenya. Muda huu wote, viongozi wa Kenya na Uganda walijaribu kuwa na mikutano kadhaa kwa lengo la kujaribu kusuluhisha. Onyango-Obbo (Feb.2017) anadai kwamba serikali za Kenya na Uganda wameshindwa kutatua mzozo huu licha ya kwamba wamekuwa na mikutano mingi tangu mwaka wa 2008.

Lugha ni mfanyiko wa kijamii ambao huuwezesha ulimwengu kuwakilishwa. Hivyo, watumiaji wa lugha huiona kama asasi yenye uwezo mkubwa katika kutekeleza majukumu mengi. Kwa mantiki hii, Diskosi au matumizi ya lugha kwa ujumla ni aina ya mifanyiko ya kijamii inayoendana na matumizi na udhihirikaji wa mamlaka, utawala, ubaguzi na upinzani. Uchunguzi wa lugha, kama inavyotumika katika jamii, husisitiza masuala yanayohusu umuhimu wa matumizi ya lugha kwa watumiaji wake. Hivyo basi, lugha ni asasi inayobebeshwa umuhimu mkubwa kiasi cha kuwapelekea wanajamii kuwekeza kwayo. Wanajamii wenyewe hutekeleza majukumu ya sampuli mbalimbali kwa kutumia lugha na, ni kutokana na mtazamo wa DHC ambapo tunafahamu namna ambavyo lugha ni mali na amali ya wanajamii husika.

Obuchi na Sangili (2016) wanadai kwamba DHC hutuwezesha kufahamu kuwa lugha hutumiwa kwa njia tofauti katika miktadha na mazingira mbalimbali. Kwa hiyo, matumizi ya lugha yanafaa kueleweka ndani ya muktadha. Ni kutokana na kauli hii

ambapo tunaweza kutambua uhusiano uliopo kati ya matumizi ya lugha na malengo yanayohusiana na matumizi hayo. Katika hali hii, tunafaa kuchunguza lugha, miundo, maumbo, pamoja na uamilifu wake kuhusiana na masuala anuwai kama vile mamlaka n.k.Wasemaji na waandishi hutekeleza majukumu yao kwa kuegemea mifanyiko ya kimaingiliano inayokitwa kwenye maslahi/malengo mahsusi yanayotawala yale ambayo yanaweza kuingizwa au kutolewa kwa diskosi husika. Kwa mfano, diskosi ya siasa, huandamana hasa na wanasiasa na taaluma ya siasa katika mapana na marefu yake (Wodak, 1989, Fairclough, 1989).

Hivyo, lengo la diskosi hii ni kuangalia namna lugha hutumiwa kwa njia tofauti katika sajili mbalimbali. Kila siku, watumiaji wa lugha hurejelea ghala kuu la maumbo ya lugha tofauti. Ghala hili linasheheni malighafi yanayowawezesha wanajamii kushiriki kikamilifu katika mawasiliano. Wanajamii hao hutawaliwa na miiko mbalimbali ambayo huwaruhusu kuwasiliana na kuingiliana kwa namna fulani. Matumizi haya yaliyokwazwa, hufungamana na masuala mbalimbali ya kiisimujamii na pia DHC. Masuala haya ni pamoja na Diskosi ya Ubaguzi wa rangi, diskosi na shughuli za uhamiaji (Van Dijk,1987; 1991; 1993). Ni kutokana na hali hii ambapo tunaelewa kwamba maingiliano ya wanajamii katika hali, shughuli na harakati mbalimbali huongozwa na misingi ya kiisimujamii. Tunahitajika kutazama matukio mbalimbali ya kimawasiliano ili kutambua namna yanaathiriwa na miundo na mifumo mbalimbali ya kilimwengu. Katika ulimwengu huu wa utandawazi, masuala mbalimbali ya kiisimujamii na pia ya diskosi changanuzi hueleweka ndani ya muktadha wa kiutandawazi. Masuala haya huweza kuhusisha shughuli za kiuchumi (Fairclough, 1995) ambazo hueleweka vizuri kwa kurejelea jamii mbalimbali ulimwenguni pasina kuzipuuzilia mbali jamii zingine. Masuala haya yanafaa kujengeka kwenye mahusiano baina ya jamii mbalimbali na namna mahusiano hayo huathiri maumbo mbalimbali ya lugha wanayoitumia kila siku, japo miundo na mifumo ya kilimwengu inasheheni utosawa.

Kisiwa hiki kimekuwa kikidaiwa na serikali ya Uganda mwaka 2008-2009 hadi 11 Mei 2009 wakati Rais Yoweri Museveni wa Uganda alikubali kuwa kisiwa hicho kipo nchini Kenya, lakini aliendelea kusema kuwa wavuvi wa Kenya walikuwa katika biashara haramu katika maji ya Uganda ambayo hupatikana mita mia chache (kama futi 700) wa magharibi wa Migingo  Bendera ya Uganda ilishushwa, askari wa Uganda waliondoka pamoja na jeshi lao, na walikubaliana kuwa afisa wa polisi wake wote wangeondoka kisiwani. Mstari wa kutenga mpaka ulizinduliwa tarehe 2 Juni 2009 ili kufidia na kuaua ardhi, ili kufanya maamuzi ya dawali ya nchi katika ziwa sahihi zaidi, na matokeo yaliyotolewa mwishoni mwa Julai 2009 kuthibitisha kwamba kisiwa kiliangukia mita kwenye upande wa Kenya. Museveni akiuanzisha mtafaruku huu alisema:

> ***Migingo Island belonged to Kenya…but the surrounding waters were Uganda has and should be treated as such.***
>
> *(Kisiwa cha Migingi ni cha Kenya…ila maji yanayokizunguka ni ya Uganda na yanastahili kuzingatiwa hivyo hivyo).*

Inabainika kuwa tamko hili la Rais Museveni lililenga kuonyesha kuwa Uganda ilikuwa na nia ya kuvua samaki wala sio kunyakua kisiwa hicho. Museveni aliendelea kusisitiza kwamba wavuvi kutoka Kenya hawangeruhusiwa kuvua samaki katika kisiwa hicho. Katika hali hii, Museveni anatumia lugha yenye kukuza mwelekeo fulani katika jamii pana na inayoendana na matumizi na udhihirikaji wa mamlaka, utawala, ubaguzi na upinzani. Uchunguzi wa lugha, kama inavyotumika katika jamii, husisitiza kauli za kibinafsi na zinazolenga katika kukuza fikra zenye kumletea faida fulani za kitaifa. Akizungumza na wanahabari kutoka shirika la BBC, Museveni aliwalaumu sana vijana wa Kenya ambao, kwa maneno yake mwenyewe alisema:

> **Taking matters too far by uprooting the railway line in Kibera and rioting over Migingo Island... Mpaka inazunguka kisiwa. So I am telling those Jaluos who were rioting na wananyoa reli …if we implementthis,hakuna mjaluo atavua samaki in this water here… it is only the Island that belongs to Kenya**.
>
> *(Kung'oa reli Kibera na kugoma kwa sababu ya Kisiwa cha Migingo ni kuvuka mipaka…Mpaka inazunguka kisiwa. Kwa hiyo nawaambia hao Mjaluo ambao wanagoma na wanang'oa reli…ikiwa tutatekeleza hili, hakuna Mjaluo atavua samaki katika maji haya hapa…ni kisiwa tu pekee yake kilichomo Kenya)Tafsiri yetu*

Matamshi haya yalimghadhabisha mbunge mmoja wa Kenya, Mheshimiwa John Mbadi ambaye alilalamika: akisema:

> **We want Kibaki to tell Museveni that his comments on the Luo are unacceptable; we can't let him bring his dictatorial tendencies into our country. Mr Museveni should not turn a national issue into a tribal issue.**
>
> *(Tunataka kumwambia Museveni kwamba matamshi yake kuhusu Wajaluo hayakubaliki; hatuwezi kumruhusu atuletee tabia zake za kidikteta katika taifa letu. Bwana Museveni hafai kugeuza suala la kitaifa kuwa la kikabila).*

Rais Museveni anafahamu fika kuwa anafaa kuwatetea Waganda kwa kuhakikisha kuwa kisiwa cha Migingo kinatambulika wazi kuwa ni milki na himaya ya nchi ya Uganda. Hivyo, anafanya kila juhudi za kuhakikisha kuwa anayatimiza malengo yanayohusiana na matarajio ya kitaifa. Katika hali hii, tunafaa kuelewa kuwa lugha, miundo, maumbo, pamoja na uamilifu wa lugha unahitajia kuhusishwa na kuhusiana na masuala anuwai kama vile turathi za kitaifa, njia za kuzalisha uchumi. Kwa mujibu wa DCH, viongozi au wanaoshiriki mazungumzo huelekeza welewa wa hisia, mawazo na dhamira ya wanajamii. Matamshi ya Rais Museveni yanadhihirisha hasira na chuki, sio tu kwa wazo la Kenya kudai kisiwa cha Migingo bali pia kwa jamii ya Wajaluo wa Kenya. Kwa kuwa katika taifa la Kenya suala la viongozi kutetea kabila lao ni la kawaida na huchukuliwa kwa kani kubwa, mijadala ya bungeni na nje ya bunge ilionyesha kwamba baadhi ya Wakenya, hasa wa jamii 'iliyotusiwa' hawawezi kuvumilia wakiona jamii yao ikikashifiwa au kutusiwa.

Rais Yoweri Museveni alikaririwa akisema kuwa amekasirishwa na jamii ya Wajaluo nchini Kenya ambao anasema kuwa wana wazimu. Rais Museveni alisema kuwa tatizo la kisiwa cha Migingo ni dogo mno kiasi cha kutosababisha uhasama kati ya nchi hizo mbili. Shirika la utangazaji la BBC, mnano tarehe 15 Mei, 2009 lilimnukuu Rais Museveni akisema kuwa Uganda ikizingatia kwa makini, sheria iliyopo, hakuna mvuvi kutoka Kenya ataruhusiwa kuvua samaki katika kisiwa hicho. Alisema kuwa mara kwa mara amekuwa akishauri **jamii ya Wajaluo wa Kenya** ambao wamekuwa wakifanya uharifu wa kung'oa reli inayoziunganisha nchi hizo mbili na kufanya maandamano kuwa hakuna mvuvi kutoka Kenya atakayeruhusiwa kuvua samaki katika maji ya kisiwa hicho. Kutokana na msimamo huo wa Rais Museveni, baadhi ya wabunge kutoka Kaunti ya Nyanza nchini Kenya wamelalamikia matamshi hayo ya Rais Museveni. Wabunge hao walimtaka Rais Kibaki kupeleka wanajeshi wa Kenya katika kisiwa hicho, na wametishia kuchukua sheria mikononi mwao ikiwa Rais Kibaki atashindwa kuchukua hatua. Rais Museveni anafahamu barabara kwamba ulimwengu huu wa utandawazi unajumuisha masuala mbalimbali ya kiisimujamii, kando na kuhusisha jamii na masuala mbalimbali yanayohusu shughuli za kiuchumi (Fairclough, 1995). Ni kwa mantiki hii ambapo viongozi kutoka nchi hizi mbili wanaelekea kuyafahamu mazingira yao, ikiwa ni pamoja na makabila au jamii tumizi lugha katika nchi jirani (Wajaluo). Kwa vyovyote, jamii hizo haziwezi kupuuziliwa mbali. Ni kutokana na mkondo huu wa mawazo ambapo vyombo vya habari vilitangaza wazi kuwa mataifa haya mawili yalifaa kuhakikisha kuwa mgogoro huo unadhibitiwa na kusuluhishwa haraka iwezekanavyo (*Daily Nation* Mei 1, 2009 ; June 20, 200 ; Septemba 25, 2009). Taarifa za gazeti la *Daily Nation* zilishapaliliwa na lile la *Daily Monitor,* ambalo huchapishwa nchini Uganda (*Daily Monitor* Oktoba 27, 2008).

Tamko la karibuni la Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, ni kwamba kisiwa hicho ni cha Kenya, lakini maji yanayozunguka kisiwa hicho ni ya Uganda. Kuna wabunge wa Kenya, hasa kutoka eneo la Nyanza, wanaotaka kuwahimiza wananchi wachukue hatua ya kukimiliki kisiwa hicho, ikiwa rais huyo wa Uganda atasitasita kuhusu jambo hilo. Mbunge wa Nyatike wakati huo, bwana Omondi Anyanga ambaye anawakilisha eneo mnamopatikana kisiwa cha Migingo, alifanya jaribio la kuanzisha mjadala bungeni kuhusiana na mtafaruku huu. Mjadala huo haukufua dafu kwani wabunge wengi walionelea kwamba si halali kutaja jina la rais wa nchi jirani bungeni. Mbunge huyo, hata hivyo, alifanikiwa kusema bungeni kuwa Rais Museveni hakupaswa kutumia lugha isiyoendana na maadili, hasa ikizingatiwa kuwa alielekea kuwalenga wanajamii wa Kenya huku mazungumzo yakiendelea kuhusiana na uwezekano wa kuwatumia masoroveya.Ni katika kipindi hiki ambapo Mheshimiwa Moses Wetangula ambaye alikuwa waziri wa mambo ya nje alisema kuwa kisiwa cha migingo kipo nchini Kenya (*East African Standard* Machi 15, 2009). Hili hapa tamko la Waziri huyo:

> **What President Museveni has said is the same thing we have been saying that the Island belongs to Kenya and we hope both sides will agree with the results of the boundary demarcation. We want to handle this issue diplomatically.**
>
> *(Kile ambacho Rais Museveni amesema ni kilekile ambacho tumekuwa tukisema kwamba Kisiwa ni cha Kenya na tunatumai kwamba pande hizi mbili zitakubaliana na matokeo ya ukaguzi wa mipaka. Tungependa kusuluhisha suala hili kidiplomasia).*

Bwana Musila, waziri msaidizi katika wizara ya ulinzi alipuuzilia mbali uwezekano wa kutumia majeshi kinyume na walivyotaka wabunge. Dondoo lililopo hapo juu limetumia neno diplomasia kwa kusema kuwa:

> **President Museveni's remarks on Migingo island had been misunderstood…the comments were not meant to offend anyone…The statement was <u>misconstrued, misunderstood and taken out of context.</u>.. the reason he made reference was the reason that they (British Broadcasting Corporation) are the ones who brought up the issue…That was the reason he made reference to Migingo.**
>
> *(Matamshi ya Rais Museveni kuhusu kisiwa cha Migingo yalieleweka vibaya…matamshi yake hayakulenga kumuudhi yeyote… lilitafakuriwa visivyo, halikueleweka vizuri na lilichukuliwa nje ya muktadha …sababu iliyomfanya kurejelea ilikuwa ni kwamba wao (Shirika la BBC) ndio waliozua suala hili…hii ndiyo sababu alirejelea Migingo).*

Kutokana na dondoo lililopo hapo juu, kumetumiwa **lilitafakuriwa visivyo, halikueleweka vizuri na lilichukuliwa nje ya muktadha**. Kauli hii inaonyesha kwamba licha ya kuwa Rais Museveni alitamka visivyo kama kiongozi wa taifa, baadhi ya wabunge wa Kenya walijaribu kuzima moto kwa kudai kwamba shirika la BBC ndilo lilikuwa na makosa kwa kutoa taarifa visivyo. Wabunge wakaitaka serikali iliadhibu taifa la Uganda haraka iwezekanavyokwa lengo la kulinda mipaka ya nchi. Wabunge wa Kenya waliyachukulia matamshi ya Museveni kuwa yenye: **chuki, uchochezi, matusi na madharau.** Mjadala uliendelea kupamba moto na wabunge wakawa mbioni katika kumsuta kiongozi huyo. Ni katika hali hii ambapo Waziri msaidizi katika wizara ya mambo ya nje bwana Richard Onyonka, alitaja kuwa wabunge walikuwa na haki ya kulalamika kuhusiana na matamshi ya Musevenilakini akawaomba wairuhusu serikali kuandaa jibu mwafaka kuhusiana na suala hilo.

Baadhi ya wabunge walionelea kuwa umoja wa mataifa na Amerika wangeingilia kati mtafaruku huu huku wakisisitiza kuwa Rais Museveni alikosea sana kwa kuiita jamii ya waluo *'wasiokuwa na akili timamu'* (Luos are mad). Walisisitiza kuwa matamshi haya yangehatarisha amani, umoja na usalama katika maeneo ya Afrika mashariki na kati. Kwa mujibu wa shirika la BBC (Mei 13, 2009), baadhi ya wabunge walionelea kuwa Rais Kibaki alikuwa na nafasi ya kumuadhibu kiongozi huyo ambaye alionekana kuendeleza siasa za kinafiki kati na baina ya makabila ya Kenya. Bwana

Khalwale alisema kuwa Rais Museveni alikuwa akieneza chuki zake huku akifahamu kuwa muungano wa Raila na Kibaki ulikuwa wenye chuki na mashaka. Mbunge wa Garsen wakati huo Danson Mungatana akaonya kwamba walikuwa wanajiandaa kwa vita lakini kwa sasa walikuwa wakiiomba serikali kuchukuwa hatua madhubuti dhidi ya taifa la Uganda ambalo, kwa maoni yao, ni taifa jeuri. Serikali isipochukua hatua hiyo, basi wabunge wangevuruga biashara za mpakani hadi pale ambapo Museveni angeomba msamaha. Hili lisipofanyika, basi Umoja wa Afrika mashariki ungekuwa hatarini.

> Kikosi maalum cha Jeshi la Uganda (SFC) chenye jukumu la kumlinda Rais Yoweri Museveni wa Uganda, kimepelekwa kwenye kisiwa chenye utata cha Migingo ili kudhibiti uvuvi haramu, mpakani mwa Uganda na Kenya.

Oluoch (2009) anaripoti kuwa Rais Museveni amekuwa akidai kwamba polisi wamekuwa wakihongwa na wavuvi kutoka Kenya, ambao walikuwa wanavua samaki wachanga, pamoja na kufanya uchafuzi katika ziwa. Kikosi hicho cha jeshi, ndicho kinasimamia ulinzi wa rais nchini Uganda na pia kuhakikisha kuwepo ulinzi imara wa wageni mashuhuri wanapozuru Uganda, na mtindo wake wa kazi unajulikana kuwa wa kukosa mahojiano wala mjadala. Hatua ya wanajeshi kulinda kisiwa cha Migingo katika ziwa Victoria, ni uamuzi wa Rais Museveni, licha ya kuwepo utata kuhusu umiliki wake, kati ya Uganda na Kenya, huku Kenya ikitaka Uganda kuondoa majeshi yake.

Kulingana na Abila (2003), kisiwa cha Migingo kinaripotiwa kuwa na utajiri mkubwa wa samaki. Ni kutokana na utajiri huu ambapo katika Mwaka 2011, Rais Museveni alisema kwamba kisiwa cha migingo kipo nchini Kenya lakini maji yanayokizunguka ni mali ya Uganda. Kisiwa kina wakazi takriban 500 hasa wavuvi na wafanyabiashara wa samaki. Eneo la Kenya lililotangazwa katika mkataba wa 1926 na Katiba ya Uganda husema kuwa eneo la Uganda hufikia "magharibi zaidi mwa Kisiwa cha Piramidi" ... huko ikiendelea kwa mstari sambamba hadi Kaskazini kufikia sehemu ya magharibi zaidi ya kisiwa cha Ilemba. Mstari unaounganisha sehemu hizo mbili hufikia magharibi mwa Migingo, kuweka kisiwa ndani ya Kenya pamoja na visiwa vya Piramidi na Usingo, kama inavyoonekana kwenye ramani inayojulikana kote tangu 1926.

## Hitimisho

Makala haya yamejadili suala zima la diskosi tepetevu ya migingo kuhusiana na mtafaruku uliozihusisha nchi mbili za Afrika mashariki, yaani, Kenya na Uganda. Makala yamejaribu kufafanua chanzo cha mgogoro huo kwa kuangazia matumizi ya lugha ya viongozi fulani wa Afrika Mashariki. Lugha hiyo ilielekea kuibua hisia kali sana kuhusiana na umiliki wa kisiwa hiki kinachozozaniwa. Kwa kuegemea nadharia ya DHC, tumejaribu kuonyesha namna matamshi ya viongozi mbalimbali yanaweza kuzua matatizo baina ya mataifa licha ya kwamba viongozi hawa wamefundishwa jinsi ya kusuluhisha migogoro kidiplomasia.

**Marejeleo**

Abila, R. O. (2003). *Fish Trade and Food Security: Are they Reconcilable in Lake Victoria?* [Online] Available at: http://www.fao.org/docrep/006/y4961e/y4961e0d.htm Accessed: 2014-01-05.

Austin J. L. (1962). *How to do Things with Words*. Cambridge: Havard University Press.

Bauman, R., & Sherzer J.(Eds) (1984). *Language in Use.* Eglewood Cliffs, N.J: Prentice Hall.

BBC (13/5-2009). *Kenyan MP's fury over Island Row* [online]Available at: http://news.bbc.co.uk/2/hi/africa/8048771.stm Accessed: 2014-01-05

*BBC News* (Afrika). (13 Mei 2009). *Wabunge Wa Kenya 'Ghadhabu Juu Ya Kisiwa Kunyongwa".*

Brown & Yule. (1983). *Discourse Analysis*. New York: Cambridge Press.

Collinge, N. E. (1990). *An Encyclopaedia of Language*. New York: Routledge.

Coulthard, M. (1977). *An Introduction to Discourse Analysis.* New York: Longman Inc.

Daily Monitor (27/10-2008). *Govt should solve island dispute with Kenya*, [online] Available at: http://www.monitor.co.ug/News/National/-/688334/754958/-/vxv22h/-/index.html Accessed: 2014-01-05.

Daily Nation (1/5-2009). *Kibaki Silence on Migingo Worrying,* [online] Available at: http://www.nation.co.ke/oped/Letters/-/440806/592870/-/ig99ym/-/index.html Accessed: 2014-01-05.

Daily Nation (20/6-2009). *Migingo: Kenyan MPs now back Kibaki,* [online] Available at: http://www.nation.co.ke/news/-/1056/613120/-/4gts2mz/-/index.html Accessed: 2014-01-05.

Daily Nation, (5/12-2012). *Voter Listing Disrupted on Disputed Migingo,* [online] Available at: http://www.nation.co.ke/counties/Voter-listing-disrupted-on-Migingo/-/1107872/1636888/-/xlohdxz/-/index.html Accessed: 2014-01-05 26.

*Daily Nation*. (Kenya), 26 Machi 2009. Retrieved on 5 Aprili 2009. *Kibaki: We will resolve Migingo*".

DailyNation. (25/9-2008). *Uganda kicks out Kenyans,* [online] Available at: http://www.nation.co.ke/news/-/1056/*474546*/-/5ga8naz/-/index.html Accessed: 2014-01-05.

Grice, H. P. (1975). Logic and Conversation. In P. Col and J. L. Morgan. (Eds.), *Speech Acts (Syntax and Semantics vol. 3)*. New York: Academic press.

Guy, C. (1997). *Discourse*. New York: Oxford University Press.

Halliday, M. A. K. (1973). *Explorations in the Functions of Language*. London: Edward Anold.

Homer-Dixon, T. F. (1999). *Environment, Scarcity, and Violence* (New Ed.). Princeton, N. J.: Princeton University Press.

http://onlinelibrary.wiley.com.ludwig.lub.lu.se/doi/10.1111/j.1467-825X.2009.02308.x/full Accessed: 2014-01-05.

http://www.independent.co.uk/multimedia/archive/00153/island-one_153042s.jpg. http://www.monitor.co.ug/artman/uploads/1/news2_9.jpg.

Iribemwangi, P. I., Mwenda, M., & Michira, J. N. (Eds.).(2013). *Ukuzaji wa Kiswahili.* Nairobi: Focus Publishers. Kenya.

LVFO (2001). *The Fisheries Management Plan for Lake Victoria* [online] Available at: http://www.lvfo.org/index.php/documents/lvfo-documents Accessed: 2014-01-05.

Matthew, R. A., & Floyd, R. (red.) (2013). *Environmental Security: Approaches and Issues* (1st Ed.). London: Routledge.

Mayoyo, P., & Otieno, E. (11 Machi 2009). Long-Standing Struggle For Migingo To Be Discussed. *Daily Nation* (Kenya), Retrieved on 5 Aprili 2009.

NTV Kenya. (2009). *Migingo Heats Up Parliament* [online] Available at: http://www.youtube.com/watch?v=DUIISQhHiko Accessed: 2014-01-05

Obuchi, S. M., & Abdulaziz, M. H. (2009). *Interactional Strategies in a Multilingual Context: Illustrative Examples from the Discourse of Bargaining*. Wissenschaftliche Studien, 38 Seiten. Grin, Germany

Obuchi, S. M. (2010). *Discourse in Interactional Contexts: A Case of Kiswahili*. Saarbruecken, Germany: VDM Verlag.

Obuchi, S. M. (2011). Topic Control in the Market Discourse. *Baraton Interdisciplinary Research Journal (BIRJ).* Eldoret: Baraton University Press.

Obuchi, S. M. (2013). Strategic Speech Acts in the Discourse of Bargaining. *Baraton Interdisciplinary Research Journal (BIRJ).* Eldoret: Baraton University Press.

Obuchi, S. M. (2013). Vyombo vya Habari na Mawasiliano katika uendelezaji wa Kiswahili. In Oluoch, Nick. "Uganda slaps work visas on Kenyans in Migingo", *The Standard* (Kenya), 7 Machi 2009. Retrieved on 5 Aprili 2009.

Olupot, M. . Ugandan settled on Migingo in 2004. *New Vision* (Uganda). Retrieved on 5 Aprili 2009.

Onyango-Obbo, C. (2017). The row over Migingo and dangerous 'law of triviality". *The Daily Nation.*

Otieno, D., & Otieno, E. (29 Machi 2009). Migingo now a different kettle of fish, *Daily Nation* (Kenya), Retrieved on 5 Aprili 2009.

Otieno, D., & Otieno, E. (28 Machi 2009). Migingo talks turn stormy, *Daily Nation* (Kenya Retrieved on 5 Aprili 2009.

Palmer, F. R. (1981). *Semantics.* New York: Cambridge University Press.

Schffrin, D. (1987). *Discourse Markers.* New York: Cambridge University Press.

Schffrin D. (1994). *Approaches to Discourse.* Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

The East African (22/11-2008). *Kenya, Uganda in tussle over Migingo island,* [online] Available at: http://www.theeastafrican.co.ke/news/-/2558/493582/-/s0njerz/-/index.html Accessed: 2014-01-05.